

13. Invisible Cities

13. Invisible Cities

Karibu kwenye muhtasari wa kitabu cha KUMI NA TATU kwenye orodha ya vitabu 100 ninavyosoma kwa siku 100.

Invisible Cities ni riwaya iliyoandikwa na Italo Calvino inayohusu hadithi za miji mbalimbali ambazo msafiri Marco Polo anamweleza mfalme wa Tartar Kablai Khan.



Kublai Khan mtawala wa Tartars anasilikiza hadithi za Marco Polo kuhusu miji mbalimbali aliyoitembelea kwenye safari zake.

Japo haamini kila anachosikia, lakini inampa matumaini hasa akizingatia gali ambayo himaya yake inapitia.

Himaya inazungukwa na maadui ambao wanashinda kwenye mapambano mbalimbali.

Lakini pia ndani ina changamoto ya rushwa kubwa na iliyokomaa.

Marco Polo anaelezea mji wa Diomira ambao una kuta zimejengwa kwa fedha, sanamu za shaba, barabara zilizojengwa kwa madini ya risasi na jogoo wa dhahabu aliye juu ya mnara na anayewika kila asubuhi.

Ni mji unaovutia sana kwa kila anayeutembelea.

Mji mwingine ni wa Isidora ambao una majengo ya ghorofa yenye ngazi za mzunguko, ambao yamerembwa na vitu kutoka baharini na wanawake wake ni warembo.

Ni mji aliokuwa anauwaza tangu akiwa kijana, ila aliutembelea akiwa mzee.

Pia kuna mji wa Dorothea, ambao una minara mikubwa ya alumini, mageti saba na majengo mazuri ya kifahari. Kwa mtu anayetoka jangwani, mji huu ni wa kuvutia.

Marco anaendelea kumwelezea Kublai miji mingine ambayo ni Zaira na Anastasia na kote anaeleza sifa za miji hiyo na jinsi inamuonesha mtu wakati uliopita na huu uliopo.

Marco anaeleza mtu akiwa porini alama anazoziona ni miti, mawe, maua, ardhi na alama mbalimbali za wanyama waliopita.

Lakini unapoenda kwenye miji, unakutana na alama ambazo zinawakilisha vitu mbalimbali.

Alama hizo zinakuwa za kuelekeza au kuonesha vitu mtu anaruhusiwa kufanya na asivyoruhusiwa kufanya kwenye eneo husika.

Anaeleza kila jengo lina alama ya kuashiria linahusu nini.

Kupitia alama mbalimbali, mji unakuwa kama kitabu ambacho mtu anaweza kukisoma na kuelewa, hata kama haelewi lugha husika.

Marco anasema kufuatia mipangilio mizuri ya miji anayoitaja na alama zake, siyo rahisi mtu kuisahau. Mtu akiitembelea hata mara moja, picha inabaki kwenye akili yake na hata usiku anaweza kuota yuko kwenye mitaa ya mji huo.

Lakini pia anaeleza jinsi baadhi ya miji hiyo mizuri ilivyokuja kuharibiwa baadaye na kilichobaki ni kumbukumbu tu kwa wale walioweza kuitembelea.

Mwanzoni ilikuwa ni vigumu kwa Kublai kumwelewa Marco Polo kwa kuwa Marco hakuwa anaijua lugha ya Tartar, hivyo alimwelezea kwa alama na vitendo.

Lakini siku zilivyokwenda, Marco aliielewa lugha na Kublai alimuelewa zaidi, huku akipata shauku zaidi ya kujionea miji hiyo anayoelezewa.



Kublai anamwambia Marco kwamba mabalozi wengine wanaosafiri wanapokuja, huwa wanampa

taarifa za vita, njaa, ukame na mengine mabaya. Ila yeye amekuwa akimpa taarifa za miji mizuri, wanatofautiana wapi?

Marco anamjibu wanatofautiana kwa kile wanachoangalia wanapofika kwenye mji. Yeye akifika anajiona kama mkaaji wa mji ule na kupata picha ya mji husika kwa wakati uliopita na siyo tu kwa wakati uliopo ambapo mji unaweza kuwa umebadilika.

Kublai anamuuliza kama safari yake ni ya kuangalia ya nyuma, Marco anamjibu ni ya kutengeneza kesho.

Marco anaeleza miji mingi ilivyo sasa siyo ilivyokuwa huko nyuma na wala siyo itakavyokuwa siku zijazo. Lakini kupitia kujua jinsi miji hiyo ilivyokuwa huko nyuma, kunaweza kumpa mtu picha ya mji unawezaje kuwa bora zaidi.

Anaeleza unapoingia kwenye mji unaweza kuona majengo yote yanafanana, ila ni mpaka uingie ndani ndiyo ubagundua kuna tofauti kubwa.

Marco anaeleza jinsi kila mji ulivyo na hadithi zake, ambapo watu huvutiwa kuitembelea kutokana hadithi wanazokuwa wamesikia.

Japo karika kuelezea miji hiyo Marco alitumia zaidi alama na vitendo, Kublai alivutiwa kusikiliza kwani alikuwa akijiona kama tayari yuko kwenye miji hiyo, akipita kwenye mitaa, akipotea na kuangalia alama mbalimbali ili kwenda vizuri.

Kadiri siku zilivyokwenda na Marco Polo kuelewa lugha ya Tartar alitumia maneno zaidi ya alama na vitendo na Kablai hakufurahia maelezo hayo kama awali.



Kublai aligundua miji ambayo Marco alikuwa anamsimulia, haikuwa inatofautiana sana.

Hivyo aliamua kuijenga upya miji hiyo kwenye fikra zake akipunguza na kuongeza vitu kwa namna anavyotaka.

Wakati Marco anaendelea kumsimulia, hakuwa anamsikiliza, alikuwa akijenga mji kwenye akili yake. Kublai anamkatisha Marco na kumwambia kuanzia sasa yeye atakuwa anamsimulia mji ulivyo, kisha Marco amjibu kama mji huo upo au haupo.

Anaanza na mji mmoja, anaweks vitu mbalimbali, kisha anamuuliza Marco kama mji huo upo. Marco anamjibu ni kama amesoma fikra zake, maana alikuwa anaenda kumsimulia mji wa aina hiyo.

Kablai anamuuliza mji huo unaitwaje na uko wapi, anamjibu mji hauna jina na hakuna unapoweza kupatikana. Anaendelea kumweleza mji ni kama ndoto, mtu anaweza kuzitengeneza atakavyo na huwa zinachochewa na tamaa na hofu.

Kablai anamjibu yeye hana tamaa wala hofu, bali anatumia fikra zake kuja na ndoto hizo. Marco anamjibu hata miji hufikiri hivyo hivyo, lakini siyo sahihi.

Marco anampa mfano wa Zobeide ambao ulitokana na ndoto ambayo watu waliipata kwa pamoja, wako kwenye mji na wanamuona mwanamke akiwa uchi, wanamkimbiza wamkamate lakini hawampati, mwisho wanaamua wajenge mji ambao mwanamke wa aina hiyo hawezi kuwatoroka.

Kablai anamwelezea Marco mji mwimwengine alioufikiria ambao upo ufukweni, anamueleza sifa zote za mji huo, kisha kumwambia akautembelee na aje kumwambia kama upo.

Marco anamjibu ataenda kuutembelea, ila hatarudi kumwambia kama upo, kwa sababu mji huo tayari upo, ila una mlango wa kuingia tu, wa kutoka haupo.



Kablai akiwa anaendelea kusikiliza hadithi za miji ya Marco anamwambia kwamba anajua miji anayomsimulia haijawahi kuwepo, haipo na haitakuja kuwepo. Anajua pia kwamba himaya yake inaaguka ni kama mzoga unaozoa na kuliwa na wadudu. Sasa kwa nini asimueleze hayo yenye uhalia badala ya kumbembelea na hadithi hizo za uongo? Kwa nini amdanganye mtawala wa Tartar?

Marco anamjibu ni kweli utawala wake una matatizo na mbaya zaidi utawala huo umeshayazoea matatizo hayo, na hilo ndiyo linamsukuma kuelezea hadithi zake, maana zinaleta tumaini jipya, kwamba mambo yanaweza kuwa bora zaidi ya yalivyo sasa.

Anaendelea kueleza pia inasaidia kuhua ukubwa wa tatizo, kwa kumpa mfano kwamba ulitaka kujua

kiwango cha giza linalokuzunguka, kaza macho yako kwenye mwanga hafifu ulio mbali. Anamwambia kujua kuhusu miji hiyo ni tumaini la mambo kuwa mazuri na kwamba furaha inawezekana tena.

Anamwambia pia asichanganye mji na maneno anayotumia kuelezea, kwa sababu maneno yake siyo ya uongo, japo vitu anavyotaja vinaweza kuwa vya uongo.

Marco anaelezea mji wa Eutropia ambao una miji mingi ndani yake, lakini ni mmoja tu unaokuwa umekaliwa kwa wakati. Wakazi wakishachoka kwenye mji waliopo, wanahamia mji mwingine, ambapo wanaanza maisha upya, kwa kubadili makazi yao, kazi wanazofanya na hata wenza wao. Na mzunguko unakwenda hivyo.

Kablai anamwambia Marco anataka aanze kufikiria miji ambayo ni ya tofauti kabisa halafu amwambie kama inawezekana.

Marco anamjibu kanuni anayoitumia kupata miji ni kifikiria mji wenye vitu vyote visivyowezekana, visivyohitajika na vinavyokinzana. Kwa kuwa mji wa aina hiyo hauwezi kuwepo, anaanza kupunguza kimoja kimoja mpaka upatikane mji unaowezekana.

👉5

Kablai anauangalia ufalme wake, umekuwa mkubwa kupitia kuangusha tawala nyingine, lakini hali ya maisha siyo nzuri, watu hawana makazi na wanakufa kwa njaa.

Anajiambia amekuza sana ufalme kwa nje, sasa ni wakati wa kuukuza kwa ndani, kwa kujenga miji ambayo amekuwa nayo kwenye ndoto zake.

Marco anaeleza mji wa Ersilia, ambapo watu hufunga kamba kati ya nyumba zao kulingana na mahusiano yao, iwe ya undugu, biashara, utawala n.k. Kamba zikiwa nyingi kiasi cha kuwa vigumu kupitika, wanahama mji huo na kwenda kuanzisha mji mwingine.

Anaelezea mji wa Baucis ambao umejengwa hewani, ili kuufikia lazima upande ngazi. Kuna nadharia tatu kwa nini mji huo haugusi ardhi, kwamba wanaichukia, wanaiheshimu na wanataka kuiacha kama walivyoikuta.

Anaelezea mji mwingine wa Leandra ambao una miungu wa aina mbili, aina ya kwanza hukaa mlangoni na aina ya pili hukaa jikoni. Miungu hiyo kwa pamoja hukosoa kila ambacho familia hufanya. Marco Polo anaeleza daraja la mji kwa kugusia kila jiwe lililopo kwenye daraja hilo.

Kublai anamuuliza ni jiwe lipi limebeba daraja hilo? Marco anamjibu daraja halijabebwa na jiwe lolote, bali kona zinazotengenezwa na mawe hayo.

Kablai anamwuliza sasa ya nini kuelezea mawe badala ya kona? Marco anamjibu bila mawe hakuna kona.

👉6

Kablai anamuelezea kuhusu mji wa ndoto yake, anampa sifa za mji huo, ambazo zinaendana na mji ambao amewahi kuutembelea, kisha anamuuliza kama amewahi kuona mji kama huo.

Marco anamjibu hajawahi kuona wala kufikiria mji wa aina hiyo.

Kablai anamwambia basi ampe maelezo ya mji mwingine, Marco anamjibu ameshamueleza miji yote anayojua.

Kablai anamwambia bado mji mmoja, ambao ni Venice, mji anaotokea Marco Polo.

Marco anamwambia miji yote ambayo amekuwa anamuelezea, anaanzia na kile anachojua kuhusu Venice.

Kablai anataka amweleze kuhusu Venice tu, jinsi ilivyo, Marco anamjibu hatamueleza, maana akishaelezea mji anausahau na hataki kusahau mji wa Venice.

Marco anaeleza kuhusu mji wa Esmeralda ambao una njia nyingi kiasi kwamba mtu hawezi kurudia njia ile ile kila mara, hivyo mji huo una siri kubwa na hauchoshi.

Marco anaeleza mji wa Adelma ambapo kila aliyemuona kwenye mji huo anafanana na mtu aliyemfahamu kwenye maisha hake ila amekufa. Anajiambia huenda ameshaona sura nyingi kiasi kwamba zinajirudia, au huenda amekuwa na yuko kati ya wafu.

Kublai anamwambia kumbe maelezo ya miji yote anayompa ametengeneza tu kwenye fikra zake. Anamwambia huenda hajawahi kusafiri mbali kama anavyojielezea.

👉7

Kublai anamwambia Marco haamini kama ametembelea miji yote hiyo ambayo anamsimulia. Marco anamjibu kumbukumbu zake ziko vizuri, popote anapotembelea, kuna vitu hasahau. Kublai anamwambia haamini amekaa na Marco kwenye bustani akisikiliza simulizi badala ya kuwa kwenye mapambano na jeshi lake. Marco anamjibu huenda hapo walipo siyo uhalisia, labda wako kwenye ndoto tu za watu wawili waliokutana. Kublai anaongeza kwamba huenda ni ombaomba wawili waliojikuta kwenye mji ulioharibiwa na wanahadithiana jinsi mji huo ulikuwa mzuri. Marco anaelezea mji wa Clarice ambao umekuwa ukiharibiwa na kupotea, kisha kufufuka tena na kuendelea. Ni mzunguko ambao umekuwa unajirudia. Anaelezea mji mwingine wa Eusapia ambao umetengeneza nakala yake chini ga ardhi ambapo mtu akifa anakaushwa kisha kupelekwa huko na kuwekwa kwa namna ya kuendelea na jukumu alilokuwa anafanya alipokuwa hai. Kama mtu alikuwa muuza duka basi mwili wake unawekwa kwenye duka. Miji hiyo miwili ni kama pacha, mmoja hai, mwingine mfu. Marco anaelezea mji mwingine wa Leonia, ambao huanza upya kila siku. Watu wanapoamka asubuhi, wanaanza siku wakiwa wapya, wanavaa nguo mpya, wanatumia vifaa vya ndani vipya, yaani kila kitu ni kipya. Vitu vya jana vinatupwa na wazoa takataka wanakuja kuvibeba na kwenda kutupwa kwenye jalala, ambalo limeshakuwa kubwa kiasi cha kutishia kuumeza mji mzima.

👉8

Kublai anafikiria njia rahisi kuweza kuijua na kuielewa miji yote iliyo kwenye himaya yake ni kupitia mchezo wa Chess. Anamwalika Marco Polo wacheze naye mchezo huo kwa lengo la kuielewa miji vizuri. Kila kete ya mchezo huo inawakilisha mji na jinsi mchezo unavyokwenda ndivyo miji hiyo inavyobadilika. Badala ya Marco Polo kwenda kwenye safari na kumletea Mfalme habari za miji mbalimbali, sasa walicheza mchezo wa chess usio na mwisho kama njia ya kuielewa miji hiyo. Marco anamwambia hakuna mji mmoja ambao mtu anaweza kuukumbuka na ukabaki hivyo. Kwa sababu unapoingia kwenye mji kwa mara ya kwanza ni tofauti na unapoondoka kwenye mji huo kwa mara ya mwisho. Na unapouona mji kwa nje, ni tofauti na unapoingia ndani. Anaelezea mji unaoitwa Thekla, mji ambao kila wakati uko kwenye matengenezo na wakazi wake wanapoulizwa kwa nini kila wakati mji uko kwenye matengenezo, wanajibu kwa sababu hawataki mji huo uanze kuharibika. Anaelezea mji mwingine unaoitwa Olinda, huu huanzia katikati ya mji na kukua kumeza mji wa zamani, kama uyoga unavyoota na kusambaa. Kublai amezamia kabisa kwenye mchezo wa Chess kiasi kwamba haweke umakini wake kwenye kitu kingine chochote. Marco anatambua hilo na kutumia kibao wanachochezea mchezo huo kuelezea miti, misitu, miji na watu. Kublai anashangazwa na uwezo wa Marco wa kumwelezea kitu vizuri kwa kutumia ubao wa mchezo wa chess.

👉9

Kublai ana atlati ambayo miji yote iliyo kwenye himaya yake pamoja na himaya jirani imechorwa. Hivyo anajiambia hategemei jipya kutoka kwa Marco kuhusu miji hiyo. Kublai anamuuliza Marco akirudi magharibi kama atawasimulia yale aliyokuwa anamsimulia yeye. Marco anamjibu kazi yake ni kuongea, lakini wanachoelewa na kukumbuka watu ni kile wanachochagua kusikia. Hivyo hata akirudia kueleza kitu kile kile kwa watu wale wale, watakachosikia

ni tofauti kila wakati.

Kublai anakubaliana naye, anamueleza kila anapokuwa anampa simulizi za miji mbalimbali, akili yake inapata picha za miji iliyoharibika, lakini ambayo itafufuka na kustawi tena.

Kublai anachukua atlas yake yenye alama za miji yote, bara kwa bara. Kisha anapima kumbukumbu ya Marco kwenye miji hiyo, Marco anaweza kuielezea miji bila kukosea.

Kablai anamwambia anaitambua miji kiurahisi kwenye atlas kuliko anapoitembelea kwa uhalisia.

Marco anamjibu vitu vingi vilivyopo kwenye atlas huwezi kuvikuta kwenye mji halisi unapoutembelea.

Kablai pia ana atlas inayoonesha miji mipya ambayo bado haijapewa majina, ni miji mikubwa na inayoonekana kujengeka sana.

Miji hiyo inaonekana kukua na kubadilika kadiri muda unavyokwenda.

Marco anaelezea mji wa Raissa ambao ni mji usio na furaha, watu wanaianza siku wakiwa wametoka kwenye ndoto mbaya na siku nzima ya kazi ni ya kisirani, kuumia na kukosea. Wanaporudi nyumbani nako mambo ni hovyoy.

Lakini kwenye mji huo huo, kila wakati utakutana na watoto ambao wanacheza kwa furaha kubwa, wakifurahia kila kinachoendelea bila kujali.

Anaelezea mji wa Cecilia, ambapo amewahi kukutana na mchungu kondoo ambaye alimuuliza huo ni mji gani. Marco akamshangaa na kumwambia unawezaje kuwa hujui uko kwenye mji wa Cecilia, mji wa kipekee kabisa.

Mchungu kondoo akamwambia kwake miji yote inafanana, hivyo hawezi kuitofautisha, ila mapori ya kulishia kondoo, hayo anayaelewa vizuri na anaweza kuyatofautisha.

Marco anamwambia yeye ni kinyume, muda wake mwingi ameutumia kwenye miji, hivyo anaijua na kuweza kuitofautisha, ila nje ya miji, hawezi kutofautisha chochote.

Kublai anamuonesha Marco miji mingine kwenye atlas yake, miji ambayo bado haijajengwa na kumuuliza amwambia ni miji ipi inaweza kujengwa.

Marco anamjibu mji wowote unaweza kujengwa, kama tu mtu ana ndoto nao.

Kablai anamwambia kila akiangalia himaya yake ni uharibifu tu anaona, haoni namna gani miji ya ndoto yake inawezekana kujengwa.

Marco anamjibu anaona uharibifu kwa sababu hicho ndiyo anachoangalia

Anamwambia kuna njia mbili za kukabiliana na uharibifu, ya kwanza ni kuukubali kiasi cha kuuzoea na hivyo haukusumbui tena, hiyo ndiyo njia wanayotumia wengi.

Njia ya pili ni kuangalia uharibifu huo huo na kutafuta kipi kizuri kinachoweza na kuangalia hicho na kisha kuchukua hatua.

👉SOMO.

Kitabu hiki kinatupa somo kubwa sana kwenye nguvu ya fikra zetu katika kujenga mambo makubwa.

Tunaweza kuitumia nguvu hii wakati wowote, hata pale mambo yanapoonekana ni magumu. Kwa kujenga fikra zilizo sahihi, pale wengine wanapoona ugumu, wewe unaona njia.

Huhitaji kulipia au kujifunza chochote ndiyo uweze kuwa na ndoto kubwa.

Wewe tengeneza ndoto zako kubwa uwezavyo, ziamini, zipambanie na utazifikia.

Muhtasari huu umeandaliwa na Kocha Dr Makirita Amani,

www.t.me/somavitabutanania